



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI



TAARIFA KWA UMMA KUHUSU WAGOMBEA WALIOTEULIWA KUWANIA  
UBUNGE NA UDIWANI KATIKA UCHAGUZI MDOGO WA JIMBO LA  
MBARALI NA KATA SITA ZA TANZANIA BARA

Dodoma, 22 Agosti, 2023

Tume ya Taifa ya Uchaguzi imeteua wagombea 58 kutoka vyama 17 vya siasa kuwania nafasi wazi ya Ubunge Jimbo la Mbarali lililopo Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali na kata sita za Tanzania Bara. Uchaguzi huo utafanyika tarehe 19 Septemba, 2023.

Jumla ya wagombea 70 walichukua fomu za uteuzi. Kati yao, wagombea 58 waliteuliwa na wagombea 12 hawakurejesha fomu za uteuzi. Hivyo, walikosa sifa ya kuteuliwa. Kati ya wagombea 58 walioteuliwa wagombea 44 sawa na asilimia 75.8 ni wanaume na wagombea 14 sawa na asilimia 24.2 ni wanawake.

Wagombea hao wametoka kwenye vyama 17 ambavyo ni; AAFP, ACT - WAZALENDO, ADA - TADEA, ADC, CCK, CCM, CUF, DEMOKRASIA - MAKINI, DP, TLP, NCCR - MAGEUZI, NLD, NRA, SAU, UDP, UMD na UPDP.

Pamoja na Jimbo la Mbarali, kata zitakazofanya uchaguzi mdogo ni; Nala iliyopo Halmashauri ya Jiji la Dodoma, Mfaranyaki iliyopo Halmashauri ya Manispaa ya Songea, Mtyangimbole iliyopo Halmashauri ya Wilaya ya Madaba, Mwaniko iliyopo Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi, Old Moshi Magharibi iliyopo Halmashauri ya Wilaya ya Moshi na Marangu Kitowo iliyopo Halmashauri ya Wilaya ya Rombo.

Tarehe 05 Agosti, 2023 Tume ilitangaza uchaguzi mdogo wa Jimbo la Mbarali na kata sita za Tanzania Bara na uteuzi wa wagombea umefanyika tarehe 19 Agosti, 2023, kampeni za uchaguzi zimeanza tarehe 20 Agosti, 2023 na zinatarajiwa kuhitimishwa tarehe 18 Septemba, 2023.

Imetolewa na:

Emmanuel Kawishe  
**KAIMU MKURUGENZI WA UCHAGUZI**